JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI

MAELEZO YA NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI
MHE. JEREMIAH S. SUMARI (MB)
WAKATI AKICHANGIA MAJUMUISHO YA WAHESHIMIWA WABUNGE KUHUSU MWONGOZO WA UTAYARISHAJI WA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA 2010/11 – 2012/13

DODOMA

TAREHE 5 FEBRUARI, 2010

MAELEZO YA NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI, MHE. JEREMIAH S. SUMARI (MB), WAKATI AKICHANGIA MAJUMUISHO YA WAHESHIMIWA WABUNGE KUHUSU MWONGOZO WA UTAYARISHAJI WA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA 2010/11 – 2012/13, DODOMA, TAREHE 5 FEBRUARI, 2010

1. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii nami kuchangia hoja kuhusu Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali wa muda wa kati 2010/11 – 2012/13 iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mhe. Mustafa Haidi Mkulo (Mb.). Awali ya yote nieleze kuwa naunga mkono hoja hiyo kwa asilimia mia moja.

2. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** baada ya maelezo hayo, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia baadhi ya hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili hoja iliyotolewa na Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi kama ifuatavyo:-

3. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu mikakati ya kutumia soko la pamoja la Afrika Mashariki katika kuinua uchumi, Mwongozo umeeleza namna ya kulitumia soko hilo pamoja na masoko mengine yatokanayo na ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda. Baadhi ya mikakati ni: Kuandaa taratibu za kisheria za kusimamia Soko la Pamoja la Afrika Mashariki; Kuandaa programu za kuhamasisha wananchi na kuwapa elimu kuhusu soko la pamoja; na Kuandaa mkakati wa kitaifa katika kutekeleza Soko la Pamoja la Afrika Mashariki ili kuhakikisha Watanzania wanafaidika na

fursa zinazotokana na soko hilo. Aidha, Tanzania itaandaa Sera ya Taifa ya ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda.

4. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, ili kuhakikisha kuwa Tanzania inapunguza gharama za kufanya biashara, Serikali inatekeleza Mradi wa Kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini (BEST) kwa kushirikisha sekta binafsi. Mradi huu unashughulikia urekebishaji wa sera na mfumo wa sheria zinazotawala mazingira ya biashara na uwekezaji. Baadhi ya mafanikio yaliyokwishapatikana katika mradi wa BEST ni pamoja na: Kukamilika kwa maandalizi ya Muswada wa Sheria ya Kusajili Shughuli za Kibiashara; Kukamilika kwa maandalizi ya sera ya kusimamia utoaji wa leseni; Kukamilika kwa maandalizi ya mradi wa Vitambulisho vya Kitaifa; na Kuwezesha kupatikana kwa 'database' ya sheria na kanuni zinazohusu biashara katika mtandao wa kompyuta popote duniani.

5. Hali kadhalika, Serikali inapitia na kufanya marekebisho ya sera, sheria na kanuni ili kupunguza gharama za kufanya biashara nchini bila kuathiri uchumi wetu hasa vyanzo vya mapato. Aidha, Kamati maalum ya Makatibu Wakuu chini ya Uenyekiti wa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu imeundwa ili kupitia na kutoa mapendekezo ya kupunguza gharama za kufanya biashara nchini. Kamati hiyo tayari imetoa taarifa yake ya awali ambayo Serikali inaifanyia kazi.

6. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu hoja ya kutumia fursa za kijiografia katika kuongeza kasi ya ukuaji uchumi, Serikali inaandaa Mpango wa Muda wa Kati wa Uwekezaji wa Umma (2010 – 2015).

Mpango huu unajumuisha kutumia fursa za kijiografia zinazoifanya Tanzania kuwa njia kuu ya usafiri kwa nchi jirani zisizo na bandari. Msukumo utawekwa katika kutumia reli, barabara pamoja na bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Kigoma kusafirisha mizigo kwenda nchi jirani. Mpango unalenga pia kufufua kiwanda cha kusafisha mafuta ghafi ya petroli, kujenga bomba kuu la mafuta kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na kuunganisha mikoa mingine na nchi jirani.

7. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kuhusu hoja ya kuongeza vyanzo vipya vya mapato ya Halmashauri, TRA itashirikiana na OWM – TAMISEMI ili kujenga uwezo wa watendaji wa Serikali za Mitaa katika kuboresha ukusanyaji wa mapato yaliyopo na kuibua vyanzo vipya katika maeneo yao.

8. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kuhusu uwezekano wa Halmashauri kukopa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo, Serikali inaandaa utaratibu utakaowezesha Halmashauri kukopa kutoka soko la mitaji la ndani kupitia mfumo wa Hatifungani za Manispaa (Municipal bonds).

9. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kuhusu ushirikishwaji wa sekta binafsi katika miradi ya maendeleo, Serikali imekamilisha Sera ya PPP na inaandaa sheria na kanuni za utekelezaji wake.

10. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia kwa kuonesha kuwa uchumi wa Taifa unaendelea kukua lakini umasikini unazidi kuongezeka hasa katika maeneo ya vijijini. Kwa

ujumla ukuaji wa uchumi ni kigezo kinachopima ongezeko katika uzalishaji wa bidhaa na huduma katika nchi katika kipindi fulani ambacho kwa Tanzania ni robo mwaka na mwaka mmoja. Umaskini nao una tafsiri nyingi kulingana na matumizi. Kwa mfano kuna baadhi ya watu wanaotafsiri umaskini kutokana na kipato cha mtu, ama wengine hutafsiri kulingana na mahitaji ya msingi ya mtu kwa siku, na pia wengine wanatafsiri umaskini kulingana na upatikanaji wa chakula kwa siku.

11. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** kuna uhusiano mkubwa kati ya kuongezeka ama kukua kwa shughuli za kiuchumi na kupungua kwa kiwango cha umaskini. Katika kipindi cha miaka ya 1990, uchumi wetu ulikua kwa wastani wa asilimia 3 kwa mwaka. Utafiti wa matumizi ya kaya wa mwaka 1990/91 ulionesha kuwa asilimia 38.6 ya watanzania walikuwa wanaishi chini ya msitari wa mahitaji ya msingi. Aidha, utafiti wa matumizi ya kaya wa mwaka 2000/2001 ulionesha kuwa asilimia 35.7 ya watanzania walikuwa wanaishi chini ya mahitaji ya msingi, wakati uchumi ulikua kwa asilimia 3.4 kati ya mwaka 1991 – 2001. Utafiti wa matumizi ya kaya wa mwaka 2007 umeonesha kuwa asilimia 33.6 ya watanzania wanaishi chini ya kiwango cha umasikini wa mahitaji ya msingi wakati uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 7.2 mwaka 2002 – 2007. Kwa matokeo hayo, kiwango cha umasikini kimekuwa kinapungua mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, kukua kwa uchumi kunaiwezesha serikali kupata mapato zaidi ambayo hutumika

kuboresha huduma za jamii na za kiuchumi ambazo ni fursa kwa mwananchi kujiongezea kipato.

12. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kuhusu suala la TRA kudhibiti utoaji wa TIN, Serikali inaandaa na kuimarisha udhibiti wa TIN kwa kuiwekea mfumo wa picha ya vidole ujulikanao kama AFIS (Automated Fingerprint Identication System). Mfumo huu una uwezo wa kuchukua picha ya vidole vya mfanyabiashara na kuweza kumtambua iwapo atarudi tena kuomba TIN nyingine. Mkakati huu utasaidia sana kuzuia uwingi wa TIN kwa mtu mmoja.

13. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kuhusu TRA kutotoa umuhimu wa kufuatilia maeneo yenye vyanzo vikubwa vya mapato kama vile eneo la Kariakoo, Serikali imekwisha bainisha maeneo hayo na inaendelea kuweka mfumo wa kufuatilia na kudhibiti ukwepaji wa mapato. Kwa mfano, Mkoa wa Dar es Salaam umegawanywa katika Ofisi tatu kwa kila Wilaya ili kuongeza nguvu ya kuwafuatilia walipa kodi kwa karibu zaidi chini ya utaratibu wa vitalu (Block Management System). Aidha TRA imejiwekea utaratibu maalum wa kukusanya taarifa kutoka kwa wadau na vyanzo mbalimbali ili zitumike katika kukokotoa kodi sahihi hususan kwenye eneo la pango, property taxes n.k. Haya yote yanafanyiwa kazi kwenye mwaka huu wa fedha na dalili za mafanikio zimekwisha anza kujitokeza kutokana na kuongeza makusanyo yaliyopatikana kwenye eneo hili.

14. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, ili kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wanaotambulika kama waadilifu (compliant Traders) wanaendelea kuwa waadilifu, TRA inaendelea kutekeleza azma hiyo kwa kufuatilia uendelevu wa uadilifu wa wafanya biashara hao. Katika kutekeleza hatua hiyo, asilimia isiyopungua tano ya bidhaa wanazoingiza nchini kwa mwaka zinakaguliwa na wafanyabiashara hao wanafanyiwa ukaguzi (Post Clearance Audit) kuhakiki "Compliance" yao kwenye utunzaji wa kumbukumbu na usahihi wa kadhia walizowasilisha Forodha. Kwa utaratibu huo, wale ambao wataonekana kupoteza uadilifu wanaondolewa.

15. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, naunga mkono hoja.